## Je, wajua mafanikio gani yalifikiwa?

- Kufanyika kwa ufunguaji wa mpaka unaotenganisha Msitu wa Hifadhi Ruvu Kusini na maeneo ya jamii wanayopakana na hifadhi hii na kufanikiwa kwa asilimia zisizopungua 75.
- Kufanyika kwa tathimini shirirkishi ya rasilimali misitu
- Kuandaliwa na kupitishwa kwa Mipango ya uendeshaji, Sheria ndogo na Rasimu za Mikataba ya makubaliano. Hii mipango imesainiwa kuanzia ngazi ya kijiji hadi wilaya.
- Mafunzo kwa kamati kuhusu namna ya kufanya doria na kutoa taarifa
- Kupungua kwa uharibifu wa msitu wa hifadhi Ruvu Kusini kuanzia mwaka 2003 hadi 2006
- Kuwepo kwa ushirikiano wa karibu kwa wadau wa Mradi wa Misitu Yetu kwa kipindi cha miaka 2001-2006.
- Kuanzia 2006,TFCG iliweza kuwezesha utekelezaji wa usimamizi wa pamoja ingawa fedha haikuwahi kutosheleza.

## Changamoto katika usimamizi wa pamoja Msitu wa Hifadhi Ruvu Kusini

- Kati ya miaka ya 2000 mpaka 2011, asilimia 40 ya msitu wa Ukanda wa Pwani umetoweka kwa uvunaji wa mkaa.
- Kutokusainiwa kwa mkataba wa makubaliano kati ya serikali na wanajamii
- Kutokuaminiana miongoni mwa wadau
- Kupungua kwa ari na ushirikiano kati ya jamii na serikali katika usimamizi wa msitu
- Kuwepo kwa makambi makubwa ya waharibifu wa msitu ndani ya msitu wa hifadhi Ruvu Kusini hususan wachoma mkaa
- Kuwepo kwa ongezeko la uharibifu ndani ya msitu wa hifadhi Ruvu Kusini
- Uvamizi wa wafugaji ndani ya msitu wa hifadhi wa Ruvu Kusini

## Hatua sita za kuzuia upoteaji wa Msitu wa Hifadhi Ruvu Kusini

Ili kuweza kurudisha ari kwa wadau katika kusimamia usimamizi wa pamoja wa misitu yafuatayo yanaweza kufanyika:

- Kusainiwa kwa mikata ya makubaliano ambayo yamechukuwa muda mrefu kwa kuzingatia sasa kuna Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania;
- Kutolewa kwa motisha ya usimamizi wa pamoja wa misitu kwa wanajamii kwa kuzingatia sera na sheria za misitu;
- Kutekeleza mipango ya uendeshaji ya usimamizi wa pamoja na kutumia sheria ili kuzuia kiasi cha msitu uliobaki;
- Kufanyike mikutano ya wadau na kujadili mapungufu yaliopo na kutafuta mikakati ya kuendelea kwa ushirikiano madhubuti;
- Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania waanze kuendelea na zoezi la kuwaondoa wavamizi wote ndani yam situ;
- Kuwepo na mikutano ya mara kwa mara ya wadau ili kujadili utekelezaji wa Usimamizi wa Misitu wa Pamoja katika msitu wa Ruvu Kusini.

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

### Kuhusu TFCG

Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania ina dira ya kuhifadhi bioanuwai ya misitu ya Tanzania. Shughuli za TFCG ni pamoja na usimamizi shirikishi wa misitu, mawasiliano na uhamisishaji, maendeleo ya jamii, uraghabishi na utafiti.
www.tfcg.org

### Kuhusu Mama Misitu

Mradi huu una dira ya kuboresha utawala wa misitu na kunufaisha wananchi. Mradi huu ni ushirika wenza kati ya Mashirika yasio ya kiserikali kumi na moja (11).
www.mamamisitu.org

# Nini tutawarithisha vizazi vijavyo: ni ardhi mbovu au msitu kwenye Hifadhi wa Ruvu kusini?





- Mpango wa Usimamizi wa pamoja wa msitu wa hifadhi Ruvu Kusini ulianza mwaka 2004.
- Mikataba ya usimamizi wa pamoja wa misitu bado haijasainiwa.
- Tangu mwaka 2000 asilimia 40 ya Misitu ya Ukanda wa Pwani imefyekwa ndani ya hifadhi.
- Tunahitaji serikali isimamie misitu ya hifadhi na mikataba ya makubaliano isainiwe kabla ya misitu yote kuharibika.

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

Mama Misitu
Tumerithi Tuwarithishe

## Usimamizi wa pamoja wa Misitu, ni nini?

Usimamizi wa pamoja wa Misitu (JFM) ni usimamizi ambao jamii inayoishi kando ya misitu ya hifadhi huingia ubia na serikali katika usimamizi na matumizi ya misitu hiyo. Usimamizi huu hufanyika kwenye ardhi ya serikali.

Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998 na Sheria ya misitu No 14 ya 2002 vinatoa uwezo kwa jamii kushiriki katika usimamizi wa misitu ya serikali.

## Kwa nini tuhifadhi Msitu wa Ruvu Kusini?

Msitu wa Hifadhi wa Ruvu Kusini ni mojawapo ya Misitu ya Hifadhi Taifa, ulioanzishwa rasmi mwaka 1979 kwa lengo la kulinda vyanzo vya maji na hifadhi ya udongo. Dhumuni jingine ni kuhifadhi bioanuwai na kama akiba ya rasilimali za misitu kwa mji wa Dar es Salaam.

Msitu huu upo ndani ya wilaya za Kibaha na Kisarawe, Mkoa wa Pwani na una ukubwa wa hekta 35,000. Msitu huu unathaminika kitaifa na kimataifa kutokana na wingi wa bioanuwai iliyopo. Mchango wake kwa jamii ni pamoja na mahitaji muhimu kama maji, mboga, nyasi na madawa. Vilele Misitu inajukumu muhimu la kurekebisha hali ya hewa na kutunza hewa ukaa.

## Historia ya usimamizi wa pamoja Msitu wa Hifadhi Ruvu Kusini

Mnamo miaka ya 2000, Mradi wa Misitu Yetu ulianzishwa chini ya program ya Utekelezaji wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa miaka mitano.

Mradi ulitekelezwa kwa ubia kati Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Chama cha Uhifadhi Wanyama Pori Tanzania (WCST) na CARE Tanzania. Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania ndio lilopewa dhamana ya kusimamia usimamizi wa pamoja wa misitu wa Ruvu Kusini kwa kuwaunganisha wadau mbalimbali

TFCG ilianza na uhamasishaji wa jamii ili wafahamu uwepo wa sera ya misitu na sheria zinazowapa nguvu ya kushiriki katika usimamizi wa pamoja wa Msitu wa Hifadhi Ruvu Kusini. Kazi ilifanywa kuanzia mwaka 2001 kwenye vijiji 8 na vitongoji viwili 2 vilivyo kando ya msitu huu.

Vijiji hivyo ni Mpiji, Bokomnemela, Soga na Kipangege kwa Wilaya ya Kibaha na vijiji vya Kifuru, Mtamba, Chakenge na Kibwemwenda pamoja na vitongoji viwili vya Kola (kijiji Kisanga) na Malangalanga (kijiji Mzenga B). Kwa pamoja vijiji hivi viliona vina kila sababu ya kushirikiana na serikali kupitia Idara ya Misitu na Nyuki (TFS).

## Je wajua mchakato uliopitia usimamizi wa pamoja wa Msitu wa Hifadhi Ruvu Kusini?

- Kupata wataalam wa misitu kutoka Idara ya Misitu na Nyuki kwa wakati huo ili wawe wawezeshaji wa zoezi zima la kuanza kwa usimamizi wa pamoja msitu wa hifadhi Ruvu Kusini,

- Kuwashirikisha wasimamizi wa msitu wa hifadhi Ruvu Kusini kwa niaba ya Idara ya Misitu na Nyuki pamoja na Halmashauri za wilaya ya Kibaha na Kisarawe ili kufanya kazi kama timu ya pamoja,

- Kuwashirikisha wanajamii kutoka kwenye vijiji na vitongoji tajwa hapo juu ili kujua nini kinatakiwa kufanyika.

- Kufanya mikutano na wadau wote walionyeshwa hapo juu ili kujua mbinu zipi zitafaa ili kuweza kufikia hatua ya usimamizi wa pamoja Msitu wa Hifadhi Ruvu Kusini zoezi lililoendeshwa na wataalam wa Idara ya Misitu na Nyuki kutoka Dar es Salaam.

- Kufanya utambuzi wa mipaka inayoweza kutumiwa na jamii katika maeneo ya usimamizi wa pamoja.



*Maandalizi ya Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu wa Hifadhi wa Ruvu Kusini mwaka 2004*



*Wangari Maathai alipotembelea msitu wa Ruvu Kusini mwaka 2008*



*Doria za pamoja katika msitu wa Ruvu Kusini mwaka 2008*



*Mikutano ya uhamasishaji kuhusu hali ya Usimamizi wa Misitu wa Pamoja mwaka 2009*



*Uvunaji haramu wa magogo katika msitu wa Ruvu Kusini mwaka 2009*